

Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) (Marekebisho) za Halmashauri ya Mji wa Kibaha

TANGAZO LA SERIKALI NA. la Tarehe 26/10/2018

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA. 290)**

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) (MAREKEBISHO) ZA
HALMASHAURI YA MJİ WA KIBAHА, MWAKA 2018**

- | | | |
|---|----|---|
| Jina na tarehe ya
kuanza
kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa madini ya ujenzi) (Marekebisho) za Halmashauri ya Mji wa Kibaha za Mwaka 2018, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ushuru wa madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Mji wa Kibaha za Mwaka 2017 Tangazo la Serikali na.423 la tarehe 13 Oktoba 2017 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| Marekebisho ya
Tangazo la
Serikali Na.
423 ya tarehe
13/10/2017 | 2. | Marekebisho yanafanyika kwa kuongeza kifungu kipywa cha 6 mbacho kitakua na vifungu vidogo sita (6).

(1) Kutakuwa na ushuru wa madini ya ujenzi yatakayochimbwa/kutoka ndani ya Eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kibaha ambao utalipwa na mnunuzi wa |

*Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) (Marekebisho) za Halmashauri
ya Mji wa Kibaha*
Tangazo la Serikali Na ... (Linaendelea.)

madini ya ujenzi kulingana na viwango viliviyowekwa katika Jedwali B la Sheria ndogo hizi.

- (2) Kutakuwa na ushuru wa madini ya ujenzi yatakayotoka/kuchimbwa nje ya eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kibaha na kusafirishwa kwa kupita ndani ya barabara za Halmashauri ya Mji Kibaha ambao utalipwa na mnunuzi wa madini ya ujenzi kulingana na viwango viliviyowekwa katika Jedwali C la Sheria ndogo hizi
- (3) Ushuru huo utakusanywa na wakala au maafisa wa Halmashauri watakaoteuliwa na Mkurugenzi kukusanya ushuru huo.
- (4) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kutoza ushuru huo katika eneo la machimbo na katika eneo lolote lililopo ndani ya mamlaka ya Halmashauri ambapo madini hayo yanasaferishwa kwenda sehemu nyingine.
- (5) Ushuru utakaotozwa katika kifungu cha 6(2) ni kwa ajili ya uharibifu wa barabara na uchafuzi wa mazingira unaofanywa na magari hayo hata kama madini hayo hayakutolewa katika machimbo yaliyopo ndani ya Mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kibaha
- (6) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kubadili viwango vya ushuru kila mwaka wa fedha kama itaonekana kuna ulazima wa kufanya hivyo na kwa kuzingatia utaratibu wa Sheria.

*Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) (Marekebisho) za Halmashauri
ya Mji wa Kibaha*
Tangazo la Serikali Na. ... (Linaendelea.)

JEDWALI B

(Chini ya Kifungu cha 6(1)

USHURU WA MADINI YA UJENZI
YAPATIKANAYO/KUCHIMBWA NDANI YA
HALMASHAURI

AINA YA GARI	KIWANGO CHA USHURU
Gari tani 1-7	3,000/= kwa tripu
Gari tani 8 na kuendelea	5,000/= kwa tripu

JEDWALI C

(Chini ya Kifungu cha 6(2)

USHURU WA MADINI YA UJENZI
YAPATIKANAYO/KUCHIMBWA NJE YA
HALMASHAURI

AINA YA GARI	KIWANGO CHA USHURU
Gari tani 1-7	1,000/= kwa tripu
Gari tani 8 na kuendelea	2,000/= kwa tripu

*Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) (Marekebisho) za Halmashauri
ya Mji wa Kibaha*

Tangazo la Serikali Na. ... (Linaendelea.)

Lakiri ya Halmashauri ya Mji Kibaha imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Mkutano wa Baraza la Halmashauri ya Mji Kibaha uliofanyika tarehe 2/5/2018.

JENIFA C. OMOLO,
*Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji
Kibaha*

L.S

LEONARD S. MLOWE,
*Mwenyekiti,
Halmashauri ya Mji
Kibaha*

NAKUBALI,

Dodoma,
4 Octoba, 2018

SELEMANI S.JAFO (MB.)
Waziri wa Nchi-or Tamisemi